



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO  
(Mawasiliano yote yafanywe kwa Mkurugenzi wa Mji)



**Kumb. Na:** MTC/I.20/2.VOL I/88

**24/03/2025**

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA  
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1))

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, ambapo jumla ya Shilingi **325,124,561.22** zimetengwa katika awamu hii. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi kwa njia ya Mfumo wa Usimamizi na Utoaji wa Mikopo (wezesha portal) kupitia tovuti: **(mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz.)**

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- i. Kikundi cha Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Makambako.
- ii. Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
- iii. Kikundi cha Wanawake/Vijana kiwe na idadi ya wanakikundi wasiopungua watano (5) na wasizidi (10) na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,

- iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali;
- v. Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na **AJIRA RASMI**, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka **18 hadi 45**.
- vi. Wanakikundi lazima wawe ni Wakazi wa kudumu toka Mitaa/Kijiji, Kata zilizopo Halmashauri ya Mji Makambako.
- vii. Wanakikundi lazima wawe na miradi/shughuli za kuongeza kipato zinazotekelezwa ndani ya Mitaa/Vijiji, kwenye Kata zilizopo Halmashauri ya Mji Makambako.
- viii. Wanakikundi lazima wawe na utaratibu wa kujiwekea akiba katika akaunti ya kikundi chao.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielekroniki (wezesha portal) (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata/Afisa Mtendaji wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo;

- i. Barua za utambaulisho wa Makazi kwa kila mwanakikundi toka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa yenye picha passport size aliyopiga hivi karibuni.
- ii. Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa,
- iii. Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo,
- iv. Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo
- v. Taarifa ya akaunti ya benki.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **23/04/2025**

**Tangazo hili limetolewa na: -**



Appia C. Mayemba

**Kaimu Mkurugenzi**

**HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO**

**MKURUGENZI**  
**HALMASHAURI YA MJI**  
**MAKAMBAKO**